Matarajio yanafikiwa?

Changamoto nne kwa Serikali, Wabunge na Wahisani

Utangulizi

Wahisani na Serikali walikutana mwezi Desemba mwaka 2010 ili kufanya mapitio ya mwaka ya utendaji wa Misaada ya Kibajeti (*General Budget Support*). Wakati wa mapitio hayo mafanikio ya mwaka uliotangulia yalijadiliwa na malengo ya mwaka unaofuata yaliwekwa. Ilitarajiwa kwamba, kama mambo yangekwenda vizuri, wahisani wangetoa ahadi za mamilioni ya dola kuchangia bajeti kupitia Hazina. Je, fedha hizi zinawawezesha Watanzania kufikia matarajio yao ya maendeleo na huduma muhimu?

Tafiti kadhaa zilizotolewa mwaka 2010 zinaonesha kwamba nchi ilipiga hatua katika baadhi ya maeneo. Pato la Taifa la mwaka *((Gross Domestic Product (GDP))* liliripotiwa kukua kwa kiasi cha asilimia 6, vifo vya watoto wachanga na watoto wadogo viliendelea kupungua, na matumizi ya vyandarua vya kuzuia mbu yanaendelea kuongezeka. Hata hivyo, Watanzania wameachwa nyuma kimaendeleo katika maeneo mengine. Katika muhtasari huu tutaangalia maeneo mawili kati ya hayo: suala la usimamizi wa rasilimali za umma na ubora wa elimu ya msingi. Kuna changamoto nyingi muhimu zinazoikabili Tanzania; tunachagua kulenga katika maeneo haya mawili kwa sababu usimamizi madhubuti wa fedha za umma unahitajika kwa lengo la kuhakikisha rasilimali zinapotumika zinaleta matokeo, na elimu bora ni muhimu katika kuendeleza rasilimali watu.

Uwazi
pata picha kamili

Muhtasari huu umeandaliwa na Uwazi-Twaweza,
iliyopo Hivos Tanzania

Uwazi, S.L.P 38342,
Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Barua pepe: info@uwazi.org. Tovuti: www.uwazi.org

Muhtasari huu ulitolewa kwa lugha ya Kiingereza
Desemba 2010 na kutafsiriwa kwa Kiswahili Aprili 2011

Kuhusu rasilimali za umma, Taftishi ya Uwazi wa Bajeti ya mwaka 2010 inaonesha kuwa mchakato wa bajeti ya Tanzania hauko wazi kiasi cha kutosha na hivyo unawaacha wananchi gizani kuhusu namna kodi wanazolipa na fedha za wahisani zinavyotumika. Vilevile, ripoti za ukaguzi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*Controller and Auditor General*) zinaonesha jinsi Serikali ilivyoshindwa kusimamia vema rasilimali za umma na kushindwa kuchukua hatua za kutosha katika kutekeleza hoja za ukaguzi. Kuhusu elimu ya msingi, tafiti zilizofanywa na Uwezo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali zinaonesha picha inayotia wasiwasi kuhusu watoto kujifunza kwa kiwango kisichokidhi, walimu kutofika mashuleni kama inavyowapasa kufanya, na rasilimali fedha kutofika mashuleni kwa mujibu wa sera.

Muundo wa Tathmini ya Utendaji (*Performance Assessment Framework*) wa Misaada ya Kibajeti unapaswa kuzingatia mafanikio na changamoto zinazoikabili Tanzania. Vivyo hivyo, Wabunge wapya waliochaguliwa wanapaswa kuyazingatia masuala haya kama sehemu ya wajibu wao wa kusimamia kwa niaba ya wananchi.

Katika muhtasari huu tunaitaka Serikali, Wabunge na Wahisani kutafakari kuhusu changamoto hizi na kuchukua hatua madhubuti kuzishughulikia. Hatimaye ufanisi wa mapitio ya mwaka ya Misaada ya Kibajeti (GBS) unahitaji upimwe si kutokana na wale walioshiriki, mijadala iliyofanyika au jinsi viashiria vya mchakato vilivyofanikiwa, bali kwa jinsi mapitio hayo yanavyochochea matumizi bora zaidi ya rasilimali za umma katika kuwajenga wananchi wenye uwezo na wanaojiamini zaidi.

Changamoto nne kwa Serikali, Wabunge na Wahisani

Changamoto ya 1: Je, ni lini wananchi wataweza kutathmini bajeti kwa makini?

Tathmini makini ya mchakato wa bajeti inayofanywa na umma wa wananchi ni kipengele muhimu katika mfumo wowote wa udhibiti na usimamizi wa matumizi ya madaraka. Tathmini makini iliyo bora inahitaji taarifa za kutosha za bajeti zipatikane kwa wakati na kuwepo njia za mashauriano baina ya wananchi, wawakilishi waliochaguliwa na watumishi wa serikali.

Kwa mujibu wa Taftishi ya Uwazi wa Bajeti *(Open Budget Survey – OBS)* ya mwaka 2010, Tanzania ina upungufu mkubwa katika nyanja hizi. Kati ya nyaraka nane muhimu za bajeti ambazo Hazina inatarajiwa kuandaa, kuchapisha na kufikisha kwa wananchi, Tanzania inaandaa nyaraka tano na kutoa kwa wananchi nyaraka tatu tu (Jedwali la 1).

Vilevile, nyaraka za bajeti zinazotolewa kwa wananchi hazina taarifa za kutosha. Alama zinazotolewa na OBS kuhusu wingi na uzamifu wa taarifa katika nyaraka hizo zinafuata madaraja/viwango vinavyooneshwa hapa chini:

A. Taarifa za kina/zinazotosheleza zinatolewa
B. Taarifa kiasi kikubwa zinatolewa
C. Baadhi tu ya taarifa zinatolewa
D. Taarifa kidogo sana zinatolewa
E. Hakuna taarifa zinazotolewa au zinatolewa kiduchu

Karibu mara zote OBS 2010 imekuwa ikizipa nyaraka za bajeti za Tanzania alama C au chini zaidi isipokuwa ripoti za ndani ya mwaka (Jedwali la 1). Kwa kuwa nyaraka nyingi zinachelewa kutolewa, uwezo wa Wabunge, wananchi na waandishi wa habari kuchunguza kwa makini taarifa zilizopo katika nyaraka hizo unapunguzwa. Hali hii inachangia kuweka mazingira ambayo kwa kiasi kikubwa yanawaacha wananchi bila kujua namna fedha za kodi wanazolipa na rasilimali zinazotolewa na wahisani zinavyotumika na hivyo kusababisha mazingira ya ubadhirifu, kutofungamana kwa vipaumbele na, na wakati mwingine, uwezekano mkubwa wa kutendeka rushwa bila kizuizi.

Jedwali la 1: Utendaji wa Tanzania katika Taftishi ya Uwazi wa Bajeti

Waraka wa bajeti	**Upatikanaji wa waraka**	**Wingi na uzamifu wa taarifa katika waraka**
Mwongozo wa awali wa bajeti	Unaandaliwa, lakini hautolewi	Hakuna taarifa
Rasimu ya bajeti kuu	Inatolewa	Baadhi ya taarifa
Bajeti iliyopitishwa	Inaandaliwa, lakini haitolewi	Hakuna taarifa
Bajeti ya Wananchi	Haiandaliwi	Hakuna taarifa
Ripoti za ndani ya mwaka	Zinatolewa	Taarifa kiasi kikubwa zinatolewa
Mapitio ya katikati ya mwaka	Hayaandaliwi	Hakuna taarifa
Ripoti ya mwisho wa mwaka	Haiandaliwi	Hakuna taarifa
Ripoti ya Ukaguzi	Inatolewa	Baadhi ya taarifa

Chanzo: Taftishi ya Uwazi wa Bajeti, (OBS, 2010)

Kuna hatua rahisi za utekelezaji ambazo Serikali, hasa Hazina na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) zinaweza kuchukua ili kurekebisha hali hii. Tunapendekeza hatua tatu ambazo iwapo zitatekelezwa, zitafanya bajeti kuwa wazi zaidi na yenye ufanisi zaidi kwa wananchi:

1. Kuhakikisha kwamba nyaraka zote muhimu za bajeti zinazotolewa na zinapatikana kwa wakati katika tovuti ya Wizara ya Fedha. Mnamo mwaka 2009/10 vitabu vya bajeti vilivyowasilishwa Bungeni vilichapishwa katika tovuti ya Bunge baada ya kuwasilishwa Bungeni. Huu haukuwa wakati mwafaka ambao ungewezesha tathmini makini ya bajeti hiyo; hata hivyo hali hii ilikuwa bora kuliko ilivyokuwa katika mwaka 2010/11 ambapo hapakuwa na taarifa yoyote iliyochapishwa kielektroni. Katika siku zijazo Hazina inapaswa kuhakikisha kuwa:

    a. Mwongozo wa awali wa bajeti na vitabu vya bajeti vinavyowasilishwa bungeni (Executive's Budget proposals) vinachapishwa katika tovuti ya Hazina mapema kabla ya kusomwa Bungeni;
    b. Vitabu vya bajeti vilivyothibitishwa vinachapishwa katika tovuti ya Hazina mara tu baada ya Bunge kupitisha bajeti;
    c. Inaanzisha na kuweka utaratibu mzuri zaidi wa hifadhi ya nyaraka za bajeti za miaka iliyopita na kuhakikisha kuwa nyaraka za miaka inayofuata zinaongezwa katika hifadhi hiyo kwa kuzingatia wakati;
    d. Inaongeza ubora wa ukamilifu na uzamivu wa taarifa katika nyaraka za bajeti inazozitoa kwa wananchi; na
    e. 'Bajeti ya wananchi' yenye kuwasilisha taarifa za bajeti kwa njia inayoeleweka kwa urahisi inaandaliwa na kutolewa kwa ushirikiano na asasi za kiraia na kusambazwa kwa wingi kwa wananchi.

2. Kuhakikisha kwamba tovuti ya taarifa za Serikali za Mitaa inakuwa na taarifa mpya, zinazowekwa mara kwa mara, na kwa wakati kulingana na matoleo ya bajeti zilizopitishwa na ripoti za utekelezaji za kila robo mwaka za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

3. Kuchapisha kalenda ya mchakato wa bajeti (ya Serikali kuu na Mamlala za Serikali za Mitaa) inayoonesha wakati nyaraka zitakapotangazwa kwa wananchi, na matukio/fursa ambazo ni wazi kwa wananchi kuweza kushiriki.

Changamoto ya 2: Ni wakati gani mapendekezo ya ukaguzi yatakapofanyiwa kazi?

Kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) anapitia maelezo ya kifedha ya Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa (*Local Government Authorities).* Ripoti za Mkaguzi zinachunguza iwapo kanuni na taratibu za manunuzi na usimamizi wa fedha zinazingatiwa. Mwaka 2010 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali alibaini kuwa Shilingi bilioni 2.6 zilitumika kwa njia zenye kuleta utata katika Wizara na Idara za Serikali na Sekritarieti za Mikoa, na Shilingi bilioni 11.2 katika Tawala za Serikali za Mitaa. Fedha hizi zilihusisha matumizi ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2008/09. Vilevile, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali alitangaza matokeo ya kaguzi tano kuhusu ubora wa huduma zinazotolewa zikilinganishwa na fedha za umma zinazotumika *(value for money audit).*

Mdhibiti Mkuu wa Serikali alidokeza kwamba imekuwa kama tabia kwa mameneja Serikalini kutojibu hoja za ukaguzi na ameonesha kutoridhishwa na kasi ndogo ya kukua kwa ubora wa usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mathalani, ni kawaida kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoshughulikia mapendekezo yanayotokana na ukaguzi, hali ambayo Mdhibiti Mkuu wa Serikali anaitazama kama ni "hali inayoakisi kukosa umakini na kutowajibika kwa upande wa Maafisa Masuuli na menejimenti" [Mdhibiti Mkuu wa Serikali, Ripoti ya Ukaguzi wa Tawala za Serikali za Mitaa ya mwaka 2008/09, uk. 121 (*tafsiri yetu kutoka ripoti ya Kiingereza)].*

Hali hii inaonekana wazi katika ongezeko la mapendekezo yasiyotekelezwa ya kaguzi zilizopita. Kati ya mwaka 2006/7 na 2008/9 kulikuwa na ongezeko la karibu mara kumi na mbili katika kiasi cha fedha zinazohusishwa na mambo ambayo hayakutatuliwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kutoka Shilingi bilioni 4.6 katika mwaka 2006/7 hadi zaidi ya Shilingi bilioni 53 mwaka 2008/9. Katika kipindi hicho hicho, hoja za ukaguzi ambazo hazikutatuliwa za Wizara na Idara za Serikali Kuu na Sekritarieti za Mikoa ziliongezeka kutoka Shilingi bilioni 64 mwaka 2006/7 (au asilimia 1.3 ya bajeti) hadi zaidi ya Shilingi trilioni 1 mwaka 2008/9 (au asilimia 15 ya bajeti yote!). Idadi ya Halmashauri, Wizara na Idara kuu za serikali zilizoshindwa kushughulikia hoja za mkaguzi pia imeongezeka zaidi ya maradufu tangu mwaka 2006/7 (Jedwali la 2).

Jedwali la 2: Mwenendo wa mapendekezo ya ukaguzi toka kaguzi zilizopita ambayo hayakutekelezwa

Ukaguzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa			Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu (Wizara/Idara/Wakala)	
Mwaka wa fedha	**Kiasi kilichohusika (TZS)**	**Idadi ya Halmashauri zilizohusika**	**Kiasi kilichohusika (TZS)**	**Idadi ya wizara/ idara/ wakala zilizohusika**
2006/07	4,643,565,831	52	64,504,129,099	17
2007/08	32,903,395,306	112	1,036,225,348,815	17
2008/09	53,463,558,647	126	1,055,460,602,544	37

Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi ya Mdhibiti Mkuu wa Serikali ya mwaka 2008/09

Mapendekezo au mambo yaliyoibuliwa na kaguzi zilizopita na ambayo hayajatatuliwa yanahitaji kushughulikiwa bila kuchelewa. Yasiposhughulikiwa, itakuwa ni ishara kuwa matumizi mabaya ya fedha za umma yanakubalika Serikalini na wala hakuna adhabu. Hatua mbili muhimu zinaweza kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa hoja za ukaguzi zinashughulikiwa bila kupuuzwa:

1. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali atangaze katika tovuti yake kumbukumbu inayosomeka kwa urahisi ya masuala yaliyoibuliwa na kaguzi katika miaka mitano iliyopita, majibu yaliyotolewa, na masuala yaliyobaki bila kushughulikiwa.

2. Serikali ifikirie kutekeleza pendekezo la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali la kutowaajiri kwa utaratibu wa ajira ya kudumu watumishi wa ngazi za juu za menejimenti (kama ilivyo sasa), badala yake ifuate mtindo wa kuajiri kwa mikataba ambayo kutolewa kwake upya kutategemea utendaji kazi unaoridhisha. Mfumo huo utaiwezesha Serikali kuwapunguza kazini watendaji wabovu na wale wasiozingatia kanuni na taratibu za usimamizi wa fedha. Mamlaka za kuajiri zikatae kuwaweka kazini maofisa wenye rekodi mbaya katika kushughulikia masuala yanayoibuliwa na ukaguzi maofisini.

Changamoto ya 3: Je, ni lini elimu itawezesha kujifunza?

Tangu mwaka 2002 viwango vya uandikishaji shuleni vimeongezeka, maelfu ya madarasa mapya yamejengwa na maelfu ya walimu wameajiriwa. Uandikishaji katika shule za sekondari na elimu ya juu pia umeongezeka. Katika kipindi hiki bajeti ya elimu imeongezeka sana, na imefikia kiasi cha sehemu moja ya tano (asilimia 20) ya matumizi yote ya Serikali. Mafanikio haya na juhudi za nchi katika elimu hivi karibuni yametambuliwa na nchi ilitunukiwa cheti cha kufanya vizuri katika Malengo ya Maendeleo ya Milenia **(***Millenium Development Goals)* jijini New York.

Lakini swali la msingi ni: Je, mafanikio haya ya upanuzi wa elimu yanawezesha watoto kujifunza? Je, watoto wa Tanzania wana uwezo zaidi katika stadi za kusoma na kufanya hesabu? Uwezo ilifanya utafiti mkubwa wa aina yake ambao ulikuwa haujapata kufanyika nchini uliohusisha watoto 42,033 wenye umri kati ya miaka 5-16. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa ingawa watoto wengi wa Tanzania wako mashuleni, wanajifunza kidogo sana. Uwezo ilipima ustadi wa watoto kwa kutumia majaribio ya ngazi ya darasa la pili katika kusoma (Kiingereza na Kiswahili) na kufanya hesabu yaliyotayarishwa kwa kuzingatia viwango vya mitaala ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Tazama sampuli za jaribio la kusoma Kiingereza katika Jedwali la 3.

Matokeo yanaonesha kwamba watoto wengi kati ya wale waliotahiniwa katika darasa la 3 hawawezi kufaulu masomo ya darasa la 2. Imeonekana kuwa:

- Wanafunzi watatu kati ya kumi ndio waliweza kusoma Kiswahili
- Mwanafunzi mmoja kati ya kumi ndio aliweza kusoma Kiingereza
- Wanafunzi wawili kati ya kumi ndio waliweza kufanya Hesabu

Vilevile, imeonekana kuwa hata inapofika wakati wa kumaliza elimu ya msingi (darasa la 7) wanafunzi wengi wanakuwa bado hawawezi kufanya majaribio ya ngazi ya darasa la 2. Kinachoonekana ni kwamba:

- Wanafunzi wawili kati ya kumi wanaomaliza elimu ya msingi bado hawawezi kusoma Kiswahli cha ngazi ya darasa la pili.
- Wanafunzi watano kati ya kumi wanaomaliza elimu ya msingi hawawezi kusoma Kiingereza.
- Mwanafunzi mmoja kati ya kumi katika darasa la saba hawezi kufanya jaribio la Hisabati.

Jedwali la 3: Jaribio la kupima stadi za kusoma Kiingereza lililotayarishwa na *Uwezo*

e n d u w f y v j	This is my cat. That dog is big. I like my school. My home is small. I have two sisters.
boy tall good best come sing take five work	Juma is living in a small village. He gets a letter once a month. The letter is from his son Musa. Musa lives in Dodoma. Juma cannot read the letters. He asks Sara to read the letters for him. a. Where does Juma live? b. What does Sara read? c. What is the name of Juma's son?

Chanzo: Je, Watoto Wetu Wanajifunza? Uwezo, 2010

Ni wazi, matokeo haya yanaonesha kuwa shule zetu hazina ubora na kwamba chombo kinachopaswa kuhakikisha ubora wa elimu katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi hakifanyi kazi yake sawasawa. Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi wa Utendaji[2] iliyotolewa karibuni na Mkaguzi Mkuu inathibitisha hoja hii. Taarifa hiyo imeonesha kwamba Programu ya Ukaguzi wa Shule katika Wizara ya Elimu imeshindwa kutimiza vema jukumu lake la kusimamia ubora wa ujifunzaji katika shule ingawa imekuwa ikiendesha ukaguzi mara kwa mara.

Hali hizi zinaonesha kuwa jibu si fedha zaidi kwa kazi ambazo zimekuwa zinafanywa na Serikali. Rasilimali zilizoongezeka pamoja na vitendea kazi havijaleta matokeo mazuri katika kujifunza, huenda kwa sababu hazitumiwi kwa namna inayofaa na hivyo kuna haja ya kubadilisha mtazamo katika mfumo mzima wa elimu kuhusu malengo ya elimu kutoka katika kutazama vitendea kazi, na badala yake kuzingatia zaidi matokeo ya ujifunzaji.

Tafiti zilizofanywa mahali pengi duniani zinaonesha kuwa kuna uhusiano mdogo kati ya ongezeko la vitendea kazi mashuleni na mafaniko ya wanafunzi katika kujifunza, na kwamba mtazamo ulio bora zaidi na unaoweza kuleta mabadiliko yanayohitajika ni ule unaohusisha kufungamanisha motisha na matokeo bora. Mfungamano huu unapokosekana, mabilioni ya fedha za umma na rasilimali za wahisani zitaendelea kutumiwa vibaya, na mamilioni ya watoto wataendelea kwenda shuleni lakini pasipo kupata stadi za kusoma na kufanya hesabu ambazo wanazihitaji ili wafanikiwe katika maisha (wawe wananchi wenye tija kwa Taifa).

Hatua tatu za msingi zinaweza kuchukuliwa ili kuhakikisha elimu katika Tanzania inafanikiwa kutimiza malengo yake:

1. Serikali inahitaji kukiri ukubwa wa tatizo la watoto kutojifunza badala ya kuficha ukweli kwa kuangalia tu mafanikio katika ongezeko la uandikishaji na kujenga majengo mapya au kupuuza matokeo ya tafiti za Uwezo. Maofisa wa ngazi za juu wawakilishi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wamehusishwa katika uundaji wa mbinu za upimaji zilizotumiwa na Uwezo toka mwanzo wa juhudi hizi, na taratibu hizi zimehakikiwa na kuthibitishwa. Serikali inapaswa kuweka malengo thabiti na mikakati ya kukuza ubora wa ujifunzaji, na kupima mafanikio kwa utaratibu unaoweza kukubalika na uchunguzi huru.

2. Programu ya Ukaguzi wa Shule ina jukumu la kuhakikisha kuna ubora wa uhakika katika elimu, lakini ushahidi unaonesha kuwa programu hiyo imeshindwa kusimamia jukumu hili. Ili kufanya kazi yake vizuri, Programu ya Ukaguzi inapaswa kuelekeza tathmini zake katika mafanikio ya mwanafunzi na kujifunza, na jinsi walimu na rasilimali zinavyofanya kazi pamoja ili kufanikisha kujifunza, kuliko kuwa na mtazamo wa kuangalia tu vitendea kazi vya elimu. Pia, ili kuhakikisha kuwa ni chombo huru na kuepuka mgongano wa maslahi, Programu ya Ukaguzi ipewe hadhi ya kuwa taasisi huru ambayo haiwajibiki moja kwa moja kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

3. Njia mojawapo inayoweza kutumika kufunganisha motisha na matokeo badala ya vitendea kazi katika kufanikisha matokeo ni kujaribu mbinu ya malipo baada ya matokeo[3] (Cash on delivery), namna ya kulipia mafanikio kutegemeana na matokeo. (Kwa mfano, wahisani wataipa serikali kiasi fulani cha fedha kwa kila mwanafunzi anayemaliza elimu ya msingi akiwa amefikia kiwango fulani cha umahiri. Rais Kikwete ameunga mkono wazo hili lakini mpaka sasa hakuna ushahidi kuwa utaratibu huu umefanyiwa kazi kwa dhati, au kwamba kuna maandalizi yoyote ya kufanyia majaribio utaratibu huu.

Changamoto ya 4: Je, ni wakati gani watoto wetu watafundishwa katika mazingira yanayofaa?

Hali duni ya mazingira ya kutolea elimu bila shaka inachangia katika kudorora kwa ujifunzaji mashuleni. Licha ya kuwapo ushahidi wa kutosha na wito wa mara kwa mara wa kutaka kubadili hali, Serikali imeendelea kufanya vibaya katika vipengele viwili: kuhakikisha kwamba walimu wanaajiriwa kwa ulingano mzuri katika maeneo yote nchini na wanafundisha, na kwamba fedha za kutosha zinafika mashuleni kwa wakati na kwa hali ya uwazi.

Takwimu Msingi za Elimu Tanzania (*Tanzania Basic Education Statistics)* zinaonesha kwamba uwiano wa wanafunzi kwa darasa nchini Tanzania katika mwaka 2010 ni wastani wa 73:1 (wanafunzi sabini na tatu kwa darasa moja). Uwiano wa mwanafunzi kwa mwalimu ni 51:1. Takwimu hizi ni za wastani na zinaficha tofauti kubwa zilizopo kati ya wilaya na shule, na kati ya madarasa katika mashule. Tathmini ya Uwezo inazionesha wazi zaidi baadhi ya tofauti hizi. Mathalani, imebaini kuwa kuna baadhi ya shule zenye madarasa yenye wanafunzi kati ya 120 na 179 (Kielelezo cha 1).

Kielelezo cha 1: Uwiano wa wanafunzi katika darasa katika wilaya sampuli za utafiti wa Uwezo



Chanzo: Utafiti wa Uwezo, 2010

Matokeo haya yanathibitishwa pia na utafiti uliofanywa na Uwazi-Twaweza miongoni mwa shule 35 za Dar es Salaam. Utafiti huu nao uliona tofauti kubwa katika uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu katika shule, kuanzia wanafunzi 14 kwa mwalimu mmoja katika shule moja hadi wanafunzi 73 kwa mwalimu mmoja katika shule nyingine.

Matatizo haya kwa kawaida yanatokana na mambo mawili. Kwa upande mmoja fedha hazifiki shuleni kama ilivyokusudiwa (fedha ni kidogo na zinachelewa kufika shuleni) na kwa upande mwingine ni kwa sababu ya usimamizi mbovu wa rasilimani za umma. Taftishi ya Kufuatilia Matumizi ya Fedha za Umma *(Public Expenditure Tracking Surveys - PETS)* wa Elimu uliofanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na wahisani unaonesha jinsi ambavyo Serikali, kinyume na sera zake, nyakati zote imeshindwa kuweka

katika bajeti yake na kupeleka katika shule ruzuku ya dola 10 za Kimarekani kwa kila mtoto aliyeandikishwa shule kwa mwaka. Katika mwaka 2008/09 ni Shilingi 4,189 tu (au dola 3 za Kimarekani) kwa kila mtoto ndizo zilipelekwa mashuleni, ambazo hazitoshi hata kununua kitabu kimoja cha kiada kwa mtoto mmoja[4.]

Matokeo haya yanaonesha kuwa wakati bajeti yote ya elimu imeongezeka, kiasi cha fedha kinachofika shuleni ni cha chini kuliko ilivyokuwa katika miaka ya mwanzoni ya maboresho ya mfumo wa elimu. PETS inaonesha pia jinsi walimu wanavyoshindwa kuwapo kazini, na hasa katika maeneo ya vijijini, hali inayosababisha maelfu ya watoto kukosa fursa za kujifunza. Mwisho, Ripoti ya Ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mikuu wa Serikali kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2008/09 inaeleza zaidi kuhusu usimamizi mbovu wa fedha za elimu ambao unasababisha rasilimali kutumiwa vibaya au kuelekezwa kwenye matumizi mengine. Kwenye ngazi ya shule, usimamizi unaonekana kuwa dhaifu kukiwa na kiwango kidogo tu cha uwazi.

Matatizo haya si kwamba hayana ufumbuzi. Hatua zifuatazo zinaweza kuchukuliwa:

1. Serikali ihakikishe kuwa ruzuku ya dola 10 za Kimarekani kwa kila mtoto wa shule ya msingi (kiasi cha Shilingi 15,000 kwa viwango vya kubadilisha fedha vya mwaka 2010) na viwango vya juu zaidi kwa shule za sekondari zinafika mashuleni zikiwa kamili na kwa wakati. Jambo hili linaweza kufanikiwa kwa kuanzisha njia rahisi, iliyo wazi zaidi ya kuhamisha rasilimali kwenda mashuleni kutoka Serikali Kuu ili rasilimali zilizotengwa zifike mashuleni kama ilivyotarajiwa. Kiwango cha ruzuku kiwekewe masharti *(ring fencing)* ili kisitumike kwa shughuli nyingine na pia ifikiriwe namna ya kuongeza ruzuku hiyo kwa njia ya kubana matumizi katika maeneo ambayo matumizi hayana tija.

2. Serikali iongeze uwazi kwa wananchi wake katika ngazi zote hadi shuleni. Sera, kiasi cha ruzuku na ulipaji wake vionekane katika mtandao na itangazwe katika vyombo vya habari, simu za mkononi na njia nyingine ili kuwezesha kila mzazi, mwalimu na mwanafunzi kujua ni kiasi gani hasa kinapaswa kutolewa, lini, na wao wafanye nini iwapo fedha hizo hazitafika shuleni kama inavyotakiwa. Serikali inaweza kuanzisha njia wazi ya taarifa inayoonesha rasilimali zinavyoelekezwa kwenye shule mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kila shilingi iliyogawiwa iweze kufuatiliwa hadi kufika katika ngazi ya shule.

3. Serikali itatue tatizo linalojirudia la uwiano usio sawa wa kuwaajiri walimu kwa kutoa motisha ili kuajiri na kubakiza walimu kazini katika maeneo yasiyopatiwa huduma za kutosha, na kwa kukuza uwazi zaidi na usimamizi. Walimu walio

tayari kufanya kazi katika maeneo ya pembezoni wanaweza kupewa posho ya ziada ya fedha. Hifadhi ya kitaifa ya taarifa za walimu wote nchini katika shule za Serikali inaweza kuanzishwa, taarifa mpya ziingizwe mara kwa mara na ziweze kupatikana. Vilevile, taarifa kuhusu mahudhurio ya walimu ziwekwe pamoja na ziweze kupatikana kwa wananchi kupitia mfumo wa njia wazi ulioelezwa hapo juu na pia kwa njia nyingine ili kuwezesha watu wenye mamlaka, vyama vya walimu na wananchi kufuatilia iwapo walimu wanafanya kazi yao.

Hitimisho

Muhtasari huu umebainisha changamoto nzito zinazoikabili Tanzania katika masuala ya usimamizi wa rasilimali na elimu ya msingi. Muhtasari ungeweza kugusia maeneo mengi zaidi lakini tumechagua kulenga katika maeneo haya kwa sababu ya umuhimu wake mkubwa kwa maendeleo, pia kutokana na lengo la kutaka kuona kwamba Muundo wa Kutathmini Utekelezaji wa Misaada ya Bajeti **(***GBS Performance Assessment Framework)* unakuwa na malengo yakinifu zaidi. Kwa kipindi kirefu Muundo huo umeshindwa kuchochea maendeleo kutokana na msisitizo wake katika viashiria vya mchakato na usiri, na tathmini za maendeleo zisizokidhi haja na zisizo na uwazi. Mapitio ya Mwaka ya Misaada ya Kibajeti kwa mwaka 2010 yanatoa fursa ya kujiwekea malengo thabiti na kuwa wazi zaidi kuhusu matokeo yaliyo muhimu kwa wananchi. Kuhusiana na jambo hili, ushiriki makini zaidi wa Wabunge ambao utaiwajibisha Serikali na wahisani kuhusu utendaji wao utakuwa muhimu pia katika kuleta mafanikio.

Rejea za ziada

Wasomaji watakaopenda kujifunza zaidi kuhusu masuala yaliyobainishwa katika muhtasari huu wanaweza kutembelea tovuti ya Uwazi (www.uwazi.org) ambapo taarifa zinaweza kupatikana kuhusu uwazi wa bajeti, ruzuku zinazotolewa na ukaguzi wa mashule. Tovuti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (www.nao.go.tz) inawasilisha ukaguzi wa thamani kwa matumizi ya fedha za umma *(value for money audits)* pamoja na taarifa za ukaguzi wa jumla. Utafiti wa *PETS* bado haujatangazwa kwa wananchi lakini ripoti yake inaweza kupatikana katika tovuti ya *Affiliated Network for Social Accountability* (www.ansa-africa.net). Taarifa zaidi kuhusu Uwezo na matokeo ya Tathmini ya ujifunzaji zinaweza kupatikana kutoka (www.uwezonet.)

Maelezo

1. Kwa ripoti kamili tazama http://www.international budget.org/files/2010 Full_Report-English.pdf
2. Tazama http://www.nao.go.tz/files/pa/SI_CAG%20Report.pdf
3. Tazama http://cgdev.org/section/initiatives/active/codaid
4. Tazama http://www.uwazi.org/index.php?i=357